**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Juni, 2015.

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(5) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha inajumuisha mafungu saba (7) ambayo ni:-

(i) Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina;
(ii) Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha;
(iii) Fungu 13- Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu;
(iv) Fungu 21- Hazina;
(v) Fungu 22 – Deni la Taifa;
(vi) Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; na

(vii) Fungu 50 – Wizara ya Fedha.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI PAMOJA NA MAAZIMIO YA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Waziri wa Fedha Mhe. Saada M. Salum (Mb) kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilifanya uchambuzi wake. Uchambuzi huo ulifanywa katika Vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Aprili na Mei, 2015 jijini Dar es salaam na Dodoma.

| Na | HOJA/AZIMIO | UTEKELEZAJI | MAONI YA KAMATI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kamati inapendekeza kwamba serikali iandae na kuwasilisha bungeni mkakati mahsusi wa kupunguza na kudhibiti viwango vikubwa vya riba vinavyotozwa na mabenki na taasisi za fedha nchini kabla ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/16. | Chini ya mfumo wa soko huria ambapo ndiyo tunaofuata, serikali haipangi wala kudhibiti (Direct control) moja kwa moja viwango vya riba. Uchambuzi unaonyesha kuwa riba za mabenki hutegemea vigezo kadhaa, ikiwa ni pamoja na mwenendo wa riba katika soko la dhamana za serikali, gharama za upatikanaji wa fedha za kukopesha (cost of funds), sifa za mkopaji, gharama za uendeshaji, matarajio ya kutorudisha mkopo (risk premium), matarajio ya mfumuko wa bei na nguvu ya ushindani katika soko.<br><br>Serikali na hasa kupitia Benki kuu inatumia vigezo hivi kuboresha mazingira ya biashara za kibenki ili kupata viwango vizuri vya riba. Serikali pamoja na benki kuu imeendelea kuboresha mfumo wa taarifa za wakopaji, kuboresha ushindani katika masoko ya fedha, kusimamia mifumo ya malipo, kuongeza uwazi katika taasisi za fedha, kuboresha madirisha ya mikopo maalum ya kilimo na nyumba na pia kuimarisha mifuko ya udhamini. Aidha, juhudi zimeendelea katika kuboresha mahakama za biashara, kutoa vitambulisho kwa watanzania na kukamilisha utaratibu wa utoaji wa hati za kimila kwa watanzania hasa waishio vijijini.<br><br>Uchambuzi unadhihilisha kuwa kwa kipindi cha takribani miaka 5 iliyopita, riba katika soko la dhamana na pia riba za mikopo kutoka mabenki zimekuwa zikipungua. Wastani wa riba za mikopo umeshuka kutoka 24% mwaka 2011 hadi 16% mwaka 2015. Aidha, tofauti kati ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja imepungua toka 9.94% mwezi machi 2005 na 4.14% disemba 2014 hadi 2.98% mwezi amchi, 2015.<br><br>Pamoja na mafanikio haya bado zipo changamoto katika masoko ya fedha ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuendelea kuzifanya riba ziendane zaidi na hali halisi ya kiuchumi. | Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kamati inaona kuwa:<br>-Madeni ya wazabuni na wakandarasi yanachangia chefuchefu (*Non Performing Loan* - NPL).<br><br>-Serikali kuendelea kukopa zaidi katika soko la ndani ambapo huchukua nafasi ya sekta binafsi.<br><br>-Serikali kuchelewa kukamilisha utaratibu wa sovereign Rating<br><br>-Benki za Serikali kukosa mtaji wa uhakika(TIB na TPB)<br><br>Bila ya kuondoa matatizo haya riba kubwa katika mabenki zitaendelea. |
| 2 | Kamati inapendekeza | Serikali inakubaliana na pendekezo la kamati la kuwasirisha mchanganuo wa | Serikali imekaidi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kwamba katika kila mwaka wa fedha serikali iwasilishe mchanganuo wa kina wa msaada na mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa, taarifa hiyo ianishe nchi wahisani, kiasi cha mkopo pamoja na vigezo na masharti kama riba, muda na masharti mengineyo. | kina kuhusu misaada na mikopo ambayo serikali inatarajia kukopa, zikiwemo taarifa za washirika wa maendeleo na kiasi cha mkopo. Mchanganuo wa ainahii hutolewa kila mwaka katika kitabu cha bajeti ya maendeleo<br><br>Serikali inaamini katika kuendesha shughuli zake kwa uwazi, ikiwemo masuala yanayohusu misaada na mikopo. Hata hivyo, ni vema kutambua kwa kuweka wazi kuna weza kuwa na athali kwani wakopeshaji wengine wanaweza kuitaka serikali kukubali masharti magumu ya mikopo tuliyokubali katika mazingira tofauti. | Azimio la Bunge na hata sababu zinazotolewa hazina mantiki<br><br>Kamati inasisitiza Azimio la Bunge litekelezwe. |
| 3 | Kitendo cha waziri kutoa amri ya kusitisha kazi za CHC huku akijua kuna Azimio la Bunge ni kuingilia uhuru na mamlaka ya Bunge lako tukufu. Serikali ilitoa notisi kuhamisha mali zote na mashauri yote ya CHC zihamishiwe kwa msajili wa Hazina. Hivyo basi, Serikali itekeleze tamko lake kuhakikisha kwamba watumishi wote waliokuwa CHC wahamishiwe kwa Msajili wa Hazina | Kwa mujibu wa sheria inayoanzisha CHC ya "*the National bank of Commerce (Reorganization and vesting of Assets and Liabilities) Act*, Na. 23 1977 kama ilivyorekebishwa, kifungu Na.5 (2) kinampa mamlaka Waziri wa fedha kusitisha shughuli za shirika mara itakapoonekana inafaa. Kwa kutumia kifungu hicho, Waziri wa fedha alihitimisha shughuli za CHC kwa kuzihamishia Ofisi ya Msajili wa Hazina.<br>Aidha, katika kuhakikisha kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina inatekeleza majukumu yake kikamilifu, watumishi 26 waliokuwa CHC wamehamishiwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuwa na uendelevu wa shughuli zilizokuwa zinatekelezwa na CHC | Wizara imekaidi Azimio la Bunge.<br><br>Amri ya Serikali No.203 inasisitiza kuwa mtu yeyote aliyekuwa mwajiriwa wa CHC atakuwa mwajiriwa wa Ofisi ya Msajiri wa Hazina.<br><br>Hivyo kitendo cha kuwaandikia barua watumishi 22 na baadae barua ya kuwafukuza hakikubaliki na nikinyume cha Amri ya Serikali.<br><br>Kamati inasisitiza kuwa Azimio la Bunge litekelezwe. |
| 4 | Serikali ianze kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi, mifukoya jamii na wakulima wa mahindi haraka yaliyofikia shilingi | Serikali ina utaratibu wa kuhakiki kwanza deni kabla ya kulipa.hadi kufikia 30 Juni, 2014 serikali ilipokea madai ya wazabuni, watumishi, na wakandarasi kutoka wizara, mikoa, idara na wakala yanayofikia shilingi trilioni 1.451. Baada ya uhakiki jumla sahihi ya madeni haya yalifikia shilingi bilioni 863.6 tu. Serikali imepanga kulipa | Kamati inaona kuwa:-<br><br>-si sahihi kuchelewesha ulipaji wa madeni kwa kisingizio cha uhakiki kwani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | trilioni 3.6 na kuleta Mpango Mkakati utakao onyesha jinsi madeni hayo yatakavyolipwa kabla ya Bunge la Bajeti la Mwaka wa Fedha 2015/2016. | madeni ya wazabuni na watumishi ya shilingi bilioni 200 kabla ya mwisho wa juni, 2015. Kiasi kitakacho baki cha shilingi bilioni 663 kitalipwa katika mwaka wa fedha 2015/16.<br>Kwa upande wa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii ikiwa ni pamoja na yaliyotokana na wastaafu wa kabla ya mwaka 1999, serikali iko katika mchakato wa kutoa hatifungani ya muda mrefu yenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 kwa mifuko hiyo kwa ajili ya madeni yaliyokwisha iva. Hatifungani hizi zitatolewa tu baada ya uhakiki kukamilika. | uhakiki unapaswa kufanyika pindi tu ankra inapowasirishwa.<br><br>-Serikali ionyeshe ni kifungu gani kitalipia Deni kiasi cha shilingi bilioni 663 katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.<br><br>-Serikali ibainishe (*i-book*) hatifungani ya muda mrefu ya shilingi trilioni 1.5 katika hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kuweza kulipia madeni ya mifuko ya jamii ikiwemo PSPF yenye deni la wastaafu wa kabla ya mwaka 1999.<br><br>-Kamati inashangazwa na kitendo cha serikali kushindwa kulipa michango ya watumishi wake katika mfuko wa PSPF (kiasi cha shilingi bilioni 140, kuanzia Februari-mei, 2015). Hii ni kinyume cha sheria (*Its statutory and first charge*) Kamati inasisitiza kuwa madeni haya yalipwe haraka. |
| 5 | Kamati inapendekeza Bunge lako tukufu liazimie kwamba serikali na taasisi zake | Utaratibu wa ununuzi unaotumiwa na taasisi mbalimbali za umma, umeainishwa katika sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2011. Miongoni mwa taratibu zilizoidhinishwa, ni pamoja na ununuzi unaofanywa na vyombo vya ulinzi na | -Wizara imekaidi Azimio la Bunge.<br><br>-Moja ya sababu zilizopelekea |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | zishindanishe zabuni za manunuzi ya sare za majeshi, shule na mshuka ya hospitali pamoja nguo zingine zinazotumia pamba kwa viwanda vya nguo vya hapa nchini. | usalama, ununuzi wa vifaa mtambuka (*common use items*) kwa kutumia mikataba maalumu (*framework contracts*) na taratibu nyingine zenye lengo la kuendeleza viwanda vya ndani.<br><br>Sheria imetamka wazi kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vitakubaliana na mamlaka ya manunuzi ya Umma (PPRA) kuhusu orodha ya vifaa vya kawaida (*non-restricted items*) ambavyo vitanunuliwa kwa kufuata utaratibu wa kawaida kwa mujibu wa sheria ya ununuzi wa umma. Vyombo hivyo vilevile vitakubaliana orodha ya vifaa visivyo vya kawaida (*restricted items*) ambavyo kwa sababu za kiusalama vitanunuliwa kwa njia maalumu. Ununuzi wa sare za jeshi ni moja ya bidhaa zilizo katika orodha ya vifaa ambavyo si vya kawaida. Ununuzi wa vifaa kama mashuka ya hospitali unapaswa kuzingatia matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma kwa kutumia mikataba maalum kama kanuni za ununuzi wa madawa na vifaa tiba zinavyoelekeza. | kushuka kwa shilingi ya Tanzania ni pamoja na manunuzi holela ya Serikali ya kununua bidhaa kutoka nje hata kwa bidhaa zinazopatikana nchini.<br><br>-Kamati inasisitiza Azimio la Bunge litekelezwe. |
| 6 | Wizara ya fedha ieleze kiasi gani cha fedha za bajeti ya 2014/15 kiepelekwa kwa wizara na halmashauri mpaka machi 2015. | Hadi kufikia Machi, 2015 Serikali ilitumia jumla ya shilingi trilioni 13.1427 kwa ajili ya utekelezaji wabajeti. Kati yakiasi hicho, shilingi trilioni 10.726.7 ni matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi trilioni 3.915.2 za mishahara, shilingi bilioni 782.3 za malipo ya riba, na shilingi trilioni 6.811.4 ni za matumizi mengineyo.<br><br>Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo Serikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi julai, 2014 hadi machi 2015, ilipanga kutumia jumla ya shilingi triloni 5.041 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi trilioni 3.5264 ni fedha za ndai, na shilingi trilioni 1.515 ni fedha za nje. Hadi kufiki Machi 2015 Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 2.416 ambapo shilingi trilioni 1.8519 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 564.1 ni fedha za nje. Mchanganuo wa fedha zilizotolewa kwenye wizara, mikoa na halmashauri umeonyeshwa kwenye kiambatisho. | Azimio la Bunge limetekelezwa. |
| 7 | Kamati imekuwa haipewi majibu ya kutosha kwa nyakati tofauti | Hoja ya kuhakiki matumizi ya fedha za mikopo iliyotolewa kwa kiwanda cha nguo cha urafiki ilikuwa inapata pingamizi kutoka kwa mwanahisa mwenza kwa | Azimio la Bunge limetekelezwa.<br><br>-Kamati inasisitiza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ilipo omba maelezo ya matumizi ya dola milioni 27 zilizokopwa toka serikali ya China kwa ajili ya uendeshaji wa kiwanda cha urafiki, Muda wote kamati imekuwa hairidhiki na majibu yanayotolewa kwamba Dola za kimarekani milioni 12 zilizobaki china kwa ajili ya kununua bidhaa kwa ajili ya kiwanda bila kuanisha bidhaa zilizonunuliwa na kuletwa kiwandani, matumizi ya dola za kimarekani milioni 15 milioni zilizobaki zilitumika kukarabati mitambo ya kiwanda bila kuainisha mitambo iliyokarabatiwa. | kipindi kirefu. Katika kikao cha wanahisa kilichofanyika tarehe 28 Machi, 2015 Serikai ya Tanzania iliwasilisha tena hoja ya kufanyika kwa ukaguzi maalum wa mtumizi ya mikopo iliyotolewa na Benki ya Exim ya China pamoja na serikali ya China.<br><br>Hoja hii ilijadiliwa na wanahisa na kukubalika kuwa, ukaguzi maalum ufanyike ili kubaini matumizi ya mikopo hiyo. Kutokana na makubaliano hayo, Ofisi ya Msajili wa Hazina tayari imewasirishwa kwa Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hadidu za rejea kwa ajili ya kuanza zoezi hilo. Ni matarajio ya Serikali kuwa zoezi la ukaguzi litakamilika ifikapo mwezi Julai, 2015. | kuwa taarifa ya ukaguzi maalum iwasilishwe kabla ya Bunge hili kuisha. |
| 8 | Kwa kuwa Serikali imeshindwa kutimiza azma yake ya kuiongezea mtaji benki ya TIB kama ilivyokubalika katika mpango wa maendeleo wa miaka 5, Serikali ikubali ombi la TIB kuiruhusu kukopa | Serikali imetenga shilingi bilioni 30 katika kifungu maalum chini ya bajeti ya Wizara ya fedha ya mwaka 2014/2015 kwa ajili ya hiyo na itatenga fedha hizo kwa mwaka ujao wa fedha.<br><br>Barua ya dhamana (*government guarantee*) ya kuiwezesha TIB kukopa zaidi ya shilingi bilioni 200 katika masoko ya ndani na nje ya nchi imekwisha andikwa kwa TIB Development bank. | Agizo la Kamati limetekelezwa na Kamati inaipongeza Serikali. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | shilingi bilioni 300 kutoka katika mifuko ya hifadhi ya Jamii ya PPF na NSSF na kwamba serikali ikubali kutenga fedha shilingi bilioni 30 kila mwaka kulipa riba ya mkopo huo kwa mfululizo kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka wa fedha 2014/15. | | |
| 9 | Kamati inashauri Serikali kuipatia benki ya TPB mtaji wa shilingi bilioni 7.5 kama walivyoomba ambapo kamati imejiridhisha na uwezo mzuri wa kiutendaji ambavyo faida inaonekana waziwazi. | Serikali imetenga shilingi bilioni 7.5 katika fungu maalum chini ya bajeti ya Wizara ya fedha kwa mwaka 2014/15 kwa ajili hiyo na zitatolewa ndani ya mwaka huu wa fedha kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha. Aidha, serikali imeruhusu TPB kutumia faida inayopatikana kwa ajili ya kuongeza mtaji. | Agizo la kamati halijatekelezwa.<br><br>-Kamati inasisitiza agizo lake litekelezwe kabla ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 haujaisha. |
| 10 | Kamati inaagiza kwamba ifikapo 31 Desemba, 2014 nafasi zote zinazokaimiwa kwenye mashirika na taasisi za Serikali ziwe zimejazwa. | Idadi ya Taasisi zenye viongozi wanaokaimu zimeendelea kupungua ambapo mpaka kufikia tarehe 27 Aprili, 2015 ni Taasisi 15 tu ambazo bado viongozi wake wanakaimu. | Agizo la kamati limetekelezwa 50%.<br><br>Kamati inasisitiza agizo lake litekelezwe kabla ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 haujaisha. |
| 11 | *Transfer pricing*: Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi sana katika eneo hili hususani katika makampuni makubwa yenye makampuni tanzu hapa | Mamlaka ya mapato mpaka sasa imeshajenga uwezo wa kutosha kwenye kitengo chake maalum kinachoshughulikia kodi za kimataifa, hata hivyo suala la kujenga uwezo ni endelevu kutokana na ukweli kwamba ziko changamoto nyingi zinazoendelea kujitokeza katika eneo la kodi za kimataifa zinazotokana na maendeleo na maendeleo ya kiuchumi, sayansi na teknolojia ambayo yanapelekea kuibuka | Agizo la Kamati limetekelezwa na Kamati inaipogeza Serikali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | nchini (*multinational companies*), mfano katika maeneo ya madini, simu mabenki, gesi na kadhalika. Aidha eneo hili limehusishwa na rushwa kubwa kati ya makampuni na watumishi wa Serikali. Pia tafiti zinaonyesha kuwa utoroshaji wa fedha nje ya nchi unachangiwa sana na *transfer mis-pricing*. Serikali itilie mkazo katika usimamizi na udhbiti wa transfer pricing ili kuhakikisha kuwa bei zinazotumika katika kampuni mama na makampuni tanzu ni bei halisi ya soko. Aidha, muda wa kushughulikia hoja sasa ni miaka mitatu tu, muda ambao ni mfupi sana, kamati inapendeeza muda huo uongezwe hadi miaka sita. | kwa mbinu mpya na za kisiasa za ukwepaji wa kodi.<br><br>Hivyo pamoja na uwezo uliokwisha jengwa katika kitengo hiki bado mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo inaendelea kujijenga uwezo zaidi ili kuwa na uweledi zaidi katika kukabiliana na mbinu hizo mpya zinazoibuka na zitakazowekeza kuibuka huko mbeleni zikiwemo changamoto kwenye eneo la gesi na mafuta.<br><br>-kutokana na kujengewa uwezo wa kutosha, kitengo hiki kimeendelea kutoa msaada wa kitaalam (*technical support*) kwa vitengo vingine vinavyoshughulikia ukaguzi mbalimbali wa kodi katika idara ya walipa kodi wakubwa (*field audit and desk audit*) pamoja na idara ya kodi za ndani. Jitihada hizo zimeonyesha ongezeko kubwa la ulipaji kodi kwa hiari (*tax compliance*) ukilinganisha na kipindi cha nyuma kabla ya kitengo hiki kuanza kazi yake rasmi. Kwa mfano taarifa za makusanyo kwa Idara ya Walipa Kodi Wakubwa kwa mwezi desemba 2014 kumekuwa naongezeko la 22.3% na idara ya kodi za ndani 17.3%; januari 2015 22.2% kwa 21.7%; februari 2015 11% kwa 13% na machi 2015 22% kwa 21.7% na tunatarajia kuwepo kwa ongezeko zaidi hadi mwisho wa mwezi wa April 2015.<br><br>Aidha, ukaguzi wa kodi (tax audit) kwa makampuni ya kimataifa yapatayo matatu uliofanyika kwa ushirikiano wa karibu na kitengo hiki uiwezesha mamlaka kutoa makadirio ya kodi (tax assessment) ya jumla ya shilingi bilioni 125.96 (shilingi 125,957,599,089) zikihusisha maeneo mbalimbali ya kodi za kimataifa ikiwemo *Transfer Pricing* (TP) na *Permanent Establishment* (PE), hata hivyo walipa kodi hao wamepinga ukokotoaji wa kodi hizo kwa mujibu wa sheria na utaratibu zilizopo kisheria na baada ya kumalizika ukusanyaji wa kodi husika utafanywa kwa mujibu wa sheria. Ukaguzi bado unaendelea kwa makampuni mengine kwa ushirikiano na kitengo hiki. Uwepo wa zana za kufanyia kazi kama vile *Transfer pricing regulations, transfer princing* | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *guidelines* na *database* zimekuwa na mchango mkubwa katika ufanisi wa kazi ya ukaguzi.<br><br>-kutokana na kukubalika kwa mapendekezo ya kuongezwa kwa muda wa kufanya ukaguzi wa kodi kwa ujumla toka miaka mitatu iliyokuwepo hadi mitano na kuingizwa katika *Tax Administration Act*, mamlaka inatarajia kuwepo kwa ufanisi mkubwa katika ukaguzi wa masuala yahusuyo transfer Princing kutokana na uhitaji wake wa muda wa kutosha katika kuyashughulikia.<br><br>-mpaka sasa mamlaka kupitia Wizara ya fedha imefanikiwa kujiunga na kuwa mwanachama wa *Global Forum*, kwa hatua hiyo mamlaka itapata fursa ya kubadirisha taarifa za kikodi na nchi wananchama katika jumuiya hiyo ya kimataifa hii itasaidia mamlaka kupata taarifa za kikodi na kuwezesha kufanya ukaguzi wenye ufanisi na kukokotoa kodi. Mamlaka pia inaendelea na mchakato wa kuimarisha upatikanaji na ubadirishaji wa taarifa za kikodi na nchi ambazo Tanzania ina mikataba kikodi pamoja na Africa Tax Administration Forum (ATAF). Aidha, mamlaka imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali inayohusu masuala masuala ya kikodi inayoendeshwa na jumuiya za nchi a OECD na CIAT.<br><br>-mamlaka kupitia idara yake Forodha na ushuru imeendelea kufanya uthibiti wa bei katika vitu vinavyoingizwa nchini (*imports*) na vinavyouzwa nje ya nchi (*exports*) katika jitihada za kuhakikisha kuwa hakuna transfer misprincing katika bei zinazotomika. Idara hii pia imeendelea kuwasiriana kwa karibu na idara ya walipa kodi wakubwa na idara ya kodi za ndani kuhusiana na bei sahihi zinazopaswa kutumika katika kuziwezesha idara hizo kukokotoa kodi sahihi. | |
| 12 | Kamati inahoji ni kwanini Serikali inaendelea kuimba wimbo ule ule wa | Tayari Serikali imeshaanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na hatua zifuatazo zimeshakamilika:-<br><br>-ofisi kwa ajili ya kuanza shuguli za benki | Azimio la Kamati limetekelezwa na Kamati inaipongeza Serikali. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kwamba uanzishwaji wa Benki ya maendeleo ya kilimo (*Tanzania Agricultural Development Bank*) umefikia hatua za mwisho lakini benki hii haianzi ikiwa ni miaka miwili sasa tangu tuelezwe kuwa taratibu zimekamilika? Kamati inauliza tatizo la kutoanza kwa benki huu ni nini? Kwa sababu kama kila kitu kimekamilika je ni nini hasa kinasubiriwa? | hiyo imeshapatikana na taratibu za matengenezo ya ndani zinaendelea;<br><br>-bodi ya wakurugenzi imeshaundwa na kuanza kazi rasmi tangu februar 2014;<br><br>-mkurugenzi mkuu na wakurugenzi w idara mbalimbali wa benki hiyo wameshateuliwa na kuajiriwa na tayari wameshaanza kazi tangu Septemba 2014;<br><br>-baadhi ya mameneja wameshaajiriwa na taratibu kuwaahiri maafisa wengine wa ngazi mbalimbali za chini zinaendelea vizuri;<br><br>-leseni ya muda ya kuanzisha benki hiyo ya maendeleo ya kilimo imeshatolewa na Benki Kuu ya Tanzania; taratibu za kukamilisha masharti ya upatikanaji wa leseni ya kudumu ya shughuli za kibenki zinaendelea. | |

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA BAJETI ILIYOIDHINISHWA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawapongeza viongozi na watendaji wa Serikali kwa jinsi walivyo toa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa Majukumu ya Kamati yametekelezwa kimilifu na kwa jinsi wanavyo simamia Wizara na Taasisi za Umma. Aidha kamati ilivutiwa zaidi na utendaji kazi wa watumishi wafuatao:-

1. Mhe. Anna Semamba Makinda, (Mb) –Spika wa Bunge la Tanzania

   Kwa kuanzisha Kamati ya Bunge ya Bajeti, na kubadili mzunguko wa Bajeti ya Nchi;

2. Sabasaba Mshingi – Mkurugenzi Mkuu TPB-Bank;

3. Peter Noni – Mkurugenzi Mkuu TIB Development Bank Ltd;

4. Abbas Talimba – Mkurugenzi Mkuu –Gaming Board of Tanzania na

5. William Olio – Mkuregenzi Mkuu – Public Pension Fund.

**Mheshimiwa Spika,** watendaji hawa wameonyesha uhodari wa hali ya juu katika kukuza na kujenga taasisi wanazozisimamia. Siku ya jumanne katika Ukumbi wa Pius Msekwa Kamati itatoa Hati za Pongezi kwa watumishi tajwa hapo juu.

## 3.1 Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi Nchini

**Mheshimiwa Spika,** kiwango halisi cha ukuaji wa uchumi kilikuwa 7.0% mwaka 2014 ikilinganishwa na 7.3 mwaka 2013, shughuli za uchumi zilizochangia ukuaji wa uchumi ni pamoja na: ujenzi (14.1%); usafirishaji na uhifadhi (12.5%); fedha na bima (10.8%); biashara (10.0%); na viwanda (9.4%); kilimo (3.4%). Kamati inaona kuwa sekta ya kilimo na viwanda ambavyo ndiyo vina ajili watanzania walio wengi zaidi ya 70% zinakuwa kwa kiasi kidogo sana na huu ndiyo uthibitisho kuwa licha ya ukuaji wa uchumi kukua kwa 7% bado hauna mahusiano ya moja kwa moja na maisha ya watanzania.

## 3.2 Kushuka kwa Thamani ya Shilingi ya Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Machi 2014 hadi Machi 2015, thamani ya shilingi ilishuka kutoka **shilingi 1629.6** hadi **shilingi 1786.3** sawa na **9.6%** katika soko la jumla na **shilingi 1631.9** hadi **shilingi1844.5** sawa na **13.0%** katika soko la rejareja kwa kila Dola moja ya Marekani.

**Mheshimiwa Spika,** hivi sasa Dola 1 ya Marekani inabadirishwa kwa wastani wa shilingi za kitanzania 2050. Hili ni anguko kubwa sana la shilingi yetu. Madhara yaliyopatikana kutokana na shilingingi ya Tanzania kushuka thamani ni pamoja na:-

- Deni la Taifa kuogezeka kutoka **shilingi trilioni 35** hadi shil**ingi trilioni 40** ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 5;

- Mikopo ya sekta binafsi iliyoko katika Dola kuongezeka thamani;

- Bidhaa na mali ghafi kupanda bei za kuagiza bidhaa nje (*imported bill*) na hivyo kusababisha mfumuko wa bei (*imported inflation*); na

- Kupunguza kasi ya uwekezaji n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwamba pamoja na sababu zingine kushuka kwa thamani ya shilingi nchini kunasababishwa na usimamizi dhaifu wa uchumi unaotokana na:-

**Moja:** matumizi holela ya Dola (*unofficial Dollarization*) ambapo shilingi ya tanzania hutumika sambamba na fedha za kigeni;

**Mbili:** kupungua kwa mapato ya mauzo nje ya nchi (*low exportation*), kukosekana kwa viwanda vya kuongeza thamani mazao na hivyo kuuza yakiwa ghafi kwa bei ndogo; katika manunuzi ya nje baada ya mafuta ya mitambo namba mbili ni mafuta ya kula, inawezekanaje nchi yenye alizeti, pamba, karanga, michikichi bado tunakuwa wanunuzi wakubwa wa mafuta ya kula?

**Tatu:** mikopo na misaada yenye masharti yakuleta wakandarasi, vifaa vya ujenzi, na bidhaa toka nchi wahisani hata kama zinapatikana nchini. Pia kusuasua kwa mikopo na misaada kwani tulitegemea kupata mikopo ya USD 800 milioni lakini hadi sasa tumepokea USD 300 milioni tu.

**Nne:** kukosekana kwa sera na usimamizi thabiti wa manunuzi kunakopelekea manunuzi holela ya

serikali mfano miradi mingi mikubwa kuwa na wazabuni na wakandarasi toka nje ambapo malipo yao hufanyika kwa dola; manunuzi ya sare za jeshi, sare za wanafunzi na shuka za mahospitali kwa kiasi kikubwa huagizwa toka nje ya nchi pamoja na kwamba tunavyo viwanda vya nguo na pamba nyingi nchini.

**Tano:** Serikali kuwa na madeni makubwa ya wakandarasi, wazabuni na mifuko ya jamii kunakopelekea shughuli za uzalishaji nchini kudolola, wafanya biashara na wawekezaji hawa wanapokopwa hushindwa kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo hupelekea kufirisika, kukosekana kwa mapato ya serikali, ajira na kuathili uchumi kwa ujumla (*These are the key economic practione*r).

**Sita:** kukosekana kwa usimamizi thabiti wa mabenki kwa kuwa kuna tofauti kubwa sana katika mabenki na maduka ya kubadirisha fedha za kigeni (sale and buy) bei ya shilingi au dolla inatofautiana katika mabenki na maduka ya

fedha pamoja na kwamba wapo katika soko moja;

**Saba:** fedha zinazotoroshwa nje ya nchi kila mwaka (*Illicit financial outflow*) ni nyingi na hivyo zinaathili thamani ya shilingi.

**Nane:** nchi kukosa mfumo mzuri wa upatikanaji wa dola kwa wahitaji wakubwa wa dola nchini kwa ajili ya kugharamia ankara zao mfano, TANESCO, MSD, TANROAD, waagizaji wa mafuta, n.k badala yake huuziwa dola katika benki za biashara kwa bei kubwa sana.

**Tisa;** kusuasua kwa mikopo na misada kutoka kwa nchi wahisani. Kwa mfano katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 tulitegemea kupata msaada na mkopo wa dola za kimarekani milioni 800, tumepata dola za kimarekani milioni 300.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia sababu hizo na nyinginezo, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue hatua mahususi ili kunusuru uchumi wa taifa.

## 2.3 Deni la taifa

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia 31 Machi, 2015, Deni la Taifa lilifikia Dola za Marekani **bilioni 19.87** sawa na shilingi **trilioni 35.70** ikilinganishwa na Dola za Marekani **bilioni 18.67** sawa na shilingi **trilioni 30.6** Machi, 2014. Kati ya kiasi hicho, Deni la Nje ni Dola za Marekani **bilioni 14.65** sawa na shilingi **trilioni 26.33** ambazo ni sawa na 73.75% ya Deni la Taifa. Aidha Deni la Ndani lilikuwa shilingi Trilioni 9.37 sawa na 26.25% ya Deni la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania katika mwezi April na Mei hadi sasa ambapo imefikia wastani wa shilingi 2050 kwa kila dola 1 ya Marekani imeathili kwa kiasi kikubwa Deni la Taifa,  deni limeongezeka kutoka shilingi **trilioni 35.7** kama ilivyokuwa 31 Machi, 2015 na kufikia shilingi **trilioni 40.73** hili ni ongezeko la shilingi **trilioni 5.03**.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonyesha kuwa Deni la Taifa linakua kwa kasi sana kwani deni lilikuwa shilingi **trilioni 21.2**, katika kipindi cha 30 Juni 2013 na kuongezeka kufikia shilingi **trilioni 40.73** Mei 2015, hiki ni kipindi cha miaka 2 tu Deni la Taifa kuongezeka karibia mara 2. Pamoja na kwamba kila mwaka, fedha hutengwa kulipa deni hili.

**Mheshimiwa Spika,** kila mwaka Serikali imekuwa ikiongeza fedha katika kulipia Deni la Taifa (CFS), mfano Mwaka wa Fedha 2014/2015 fedha iliyotengwa kulipia Deni la Taifa ilikuwa ni shilingi **trilioni 4.35** lakini fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni shilingi **trilioni 6.39** sawa na ongezeko la shilingi **trilioni 2.04**. Hali hii inaashiria hatari kubwa kwa mapato ya usoni na mustakabali wa uchumi wa Taifa letu. Nilazima ukopaji wetu uzingatie vipindi vya kuiva kwa madeni vipindi vya nyuma.

**Mheshimiwa Spika,** ni lazima Taifa litizame upya mwenendo wa ukopaji na ukuaji wa Deni la Taifa kuliko kung'ang'ana na vigezo vya kimataifa kuwa deni la Taifa linahimilika. Malimbikizo ya riba

ni makubwa sana na hii inaashiria kwamba tunachukua mikopo yenye riba kubwa sana. Mfano malipo ya mikopo ya nje kuishia Machi ilikuwa shilingi **bilioni 429.285** wakati *principal repaid* ilikuwa shilingi **bilioni 146.856** tu, huku *interest paid* ilikuwa ni shilingi **bilioni 282.428.** Katika kipindi hicho malipo ya Deni la Ndani yalikuwa shilingi **trilioni 1.68** huku malipo ya riba yakiwa shilingi **bilioni 527.28**.

## 2.4 Usambazaji wa Fedha (*DIsbursement of Funds*)

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kutoka Wizara, Taasisi na Halmashauri kuwa utoaji wa fedhanzilizoidhinishwa na Bunge ni wakusuasua kiasi cha kuathili utekelezaji wa bajeti. Kamati ililazimika kuomba taarifa ya usambazaji wa fedha ili kujua kama mapato ya Serikali yalipatikana kama yalivyopangwa, kama fedha inatolewa kwa wakati na kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa vielelezo vilivyotolewa mbele ya Kamati zinaonyesha kuwa

katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 fedha zilizokuwa zimelipia Deni la Taifa ni shilingi **trilioni 2.636** tu wakati taarifa ya utoaji fedha (*fund disbursement*) inaoyesha kuwa fedha zilizokuwa zimetolewa katika kipindi hicho ni shilingi **trilioni 4.123** ikiwa ni tofauti ya shilingi trilioni **1.5**, Kamati inaitaka **Serikali kulieleza Bunge kiasi hiki cha shilingi trilioni 1.5 kililipwa wapi na kwa kazi gani na kama fedha hizo ziliidhinishwa na Bunge?**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuishia Machi 2015 kiasi kilichotakiwa kulipwa katika Deni la Taifa ni 75% lakini hadi kufikia kipindi hicho Serikali ilikuwa imelipa 95% ya kiasi kilichotengwa mwaka huo shilingi **trilioni 4.348**. Aidha, katika kifungu cha 7 Ofisi ya Msajili Hazina ilikuwa imepangiwa kutumia shilingi **bilioni 87.59** lakini hadi kufikia Machi 2015 walikuwa wametumia shilingi **bilioni 172.45** sawa na **197%.**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 61, Tume ya Uchaguzi ilipangiwa kutumia shilingi **bilioni 2.85** lakini hadi kufikia Machi 2015 ilikuwa imetumia **142.2** sawa na **490%.** Kamati inaona huu si

utaratibu mzuri wa kupanga na kutumia fedha za umma. Huku matumizi ya fedha za maendeleo kutoka Julai-Machi 2015 ni 28% tu.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia matumizi hayo holela ya fedha za umma, Kamati ina muagiza CAG kufanya ukaguzi maalum Hazina ili kubaini fedha hizi zimetumikaje

2.5 Mwenendo wa ukusayaji mapato na matumizi ya serikali.

Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yalikuwa shilingi **bilioni 8,184.1** (67%) ya makadirio ya Mwaka wa Fedha. Mapato haya yalikuwa chini kwa kiasi cha shilingi **bilioni 949.5** kwa kipindi hicho. Kamati ina wasiwasi kwamba kitendo cha kupandisha mapato kutoka shilingi **trilioni 12.18** (2014/2015) hadi shilingi **trilioni 14.3** (2015/2016) ikiwa ni ongezeko la **shilingi trilioni 2.12**. Kamati inajiuliza Serikali itawezaje kukusanya shilingi trilioni 14.3 wakati kuna dalili zote kuwa haitaweza kukusanya trilioni 12.18 za mwaka unaoishia sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwa mapato ya mashirika na taasisi za umma hayajaingizwa kwenye bajeti kuu kama ambavyo Bunge na Serikali tulivyokubaliana kuwa tutakuwa na *comprehensive budget* ambayo itajumuisha mapato yote ya ya Serikali. Kwa mujibu wa uchambuzi wa bajeti umeonyesha kuwa jumla ya taasisi 186 zina bajeti ya shilingi **bilioni 8,583.8**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa makisio ya bajeti ya mwaka 2015/2016, gharama za kulipia Deni la Taifa zimeongezeka toka shilingi **trilioni 4.35** (2014/2015) hadi shilingi **trilioni 6.39** (2015/2016) ongezeko la trilioni 2. Mishahara toka **trilioni 5.32** (2014/2015) hadi **trilioni 6.6** ongezeko la **trilioni 1.28**. Gharama za kulipia Deni la Taifa na mishahara zimefikia kiasi cha shilingi **trilioni 13**, ambayo inameza mapato yetu yote ya ndani.

### 2.6 Mfuko wa Uwezeshaji Uagizaji bidhaa toka nje ya Nchi (*Commodity Import Support*-CIS)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka 1980 mpaka 1992/93, Serikali ilikumbwa na uhaba mkubwa wa fedha za kigeni, kutokana na matatizo

ya kiuchumi. Washirika mbalimbali wa maendeleo walitoa fedha za kigeni kwa mpango maalum uliofahamika kama "*Commodity Import Suport-CIS*" ukilenga kuipatia Serikali uwezo wa kuimarisha uchumi wa nchi kwa kuzipatia Taasisi za Serikali, makampuni binafsi, viwanda, na wafanyabiashara mbalimbali uwezo wa kuagiza bidhaa na mali ghafi toka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha za *Commodity Import Support*-CIS zilitolewa kama mkopo ambapo wakopaji walitakiwa kulipa deni bila kutozwa riba ndani ya kipindi cha miezi 18 na baada ya hapo walipaswa kulipa riba ya 12%. Jumla ya taasisi za Serikali, makampuni binafsi, viwanda na wafanyabiashara mbalimbali zaidi ya 980 walinufaika na mikopo ya *Commodity Import Support-CIS* iliyotolewa katika nyakati mbalimbali. Katika kipindi hicho jumla ya mikopo yenye thamani ya fedha za kijapani **(JPY) 22.1 bilioni** sawa na **shilingi bilioni 328** zilizotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kabla mteja hajaruhusiwa kutumia mkopo, alitakiwa kufuata utaratibu ufuatao:-

- Kulipia 30% ya mkopo (*cash cover*) alioupata kama malipo ya awali, baada ya kulipia 30% mteja alitakiwa kuingia katika mkataba wa deni na hazina na

- Alitakiwa awasilishe taarifa kuhusu "*repayment schedule*" ya 70% ya deni lililobaki, muda wa malipo usizidi miezi kumi na nane (18).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Julai, 2013 jumla ya fedha za kijapani **JPY 6.4 bilioni** sawa na **shilingi bilioni 95.1** zilikusanywa toka kwa wadaiwa mbalimbali na kubakiwa na bakaa ya deni ya fedha za kijapani **JPY 15.7** sawa na **shilingi bilioni 233**. Kamati katika uchambuzi wake imebaini kuwa:-

**Moja:** madeni haya ni ya muda mrefu kati ya miaka 13 hadi 22, taasisi za Serikali, makampuni binafsi, viwanda na wafanyabiashara hawakulipa madeni yao kwa mujibu wa mikataba.

**Mbili:** kiasi cha bakaa ya deni kilicholipotiwa cha shilingi bilioni 233 hakijazingatia malimbikizo ya riba (*compounded interests*). Licha ya mikataba kuwa wazi kuwa baada ya miezi 18 kutatozwa riba ya 12%.

**Tatu:** baadhi ya wadaiwa wa makampuni binafsi, viwanda na wafanya biashara wameripotiwa kuwa hawapatikani wakati wapo na wanaendelea na biashara.

**Nne:** wadaiwa wengine walipewa mkopo (*amount utilised)* mkubwa zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa (*allocated amount*).

**Tano:** ukusanyaji dhaifu wa madeni haya, wadaiwa kulipa kwa kusuasua na wengine kukaidi kulipa madeni haya licha ya kuwa wanao uwezo na wana dhamana ambazo zinaweza kufilisiwa kulipia madeni yao.

**Sita:** ukusanyaji wa madeni umesimama tangu Desemba 2012 kutokana na mkataba wa *broker Msolopa Investment Co.Ltd* kufika mwisho hivyo tangu kipindi hicho hakuna jitihada zozote za ukusanyaji wa madeni hayo.

**Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa kwa wastani wa miaka 15 ya madeni haya kwa riba ya 12% deni hili hadi sasa linakadiriwa kufikia shilingi trilioni 1.4.**

***(A=P (1+r/n)*** $^{nt}$

Jedwali lifuatalo linaonyesha mfano wa kampuni zenye uwezo wa kulipa madeni hayo lakini wamekuwa wakilipa kwa kusuasua:- (Yen 1=shilingi 14.84)

| No | Jina la kampuni | Kiasi kilichokopwa | Kiasi kilicholipwa(JPY) | Kiasi kinacho daiwa (JPY**)** | Kiasi kinachodaiwa katika TSH | Compounding interestinTSh |
|---|---|---|---|---|---|---|
| i | Appolo Freight carriers | 34,236,748 | 9,356,149 | 25,180,599 | 373,680,089.16 | 2.24 bilioni |
| 2 | Farm Equip (T)Ltd | 34,236,748 | 8,922,454 | 25,314,294 | 375,664,133.96 | 2.25 bilioni |
| 3 | DSM cottage Industries | 90,688,754 | 54,530,419 | 36,158,335 | 536,589,691.4 | 3.22 bilioni |
| 4 | Quality Group Garage | 87,143,474 | 10,622,817 | 76,520,657 | 1,135,566,549.88 | 6.81 bilioni |
| 5 | Sabira Investment | 73,760,374 | 499,280 | 73,261,094 | 1,087,194,634.96 | 6.52 bilioni |
| 6 | African Trade Development | 72,842,610 | 14,194,291 | 58,648,319 | 870,341,053.96 | 5.22 bilioni |
| 7 | Dun Hill Motors | 134,618,355 | 32,281,858 | 102,336,477 | 1,518,672,873.48 | 9.11 bilioni |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | 21st centuries Textile Industries LTD | 51,617,119 | 15,000,000 | 36,617,119 | 543,398,045.96 | 3.26 bilioni |
| 9 | Universal Electronic and Hardware | 159,616,352 | 54,899,004 | 104,717,343 | 1,554,005,370.12 | 9.32 bilioni |
| 10 | Mohammed Interprices | 20,000,000 | 0 | 20,000,000 | 296,800,000 | 1.78 bilioni |
| 11 | ALAF | 200,804,406 | 50,512,841 | 150,291,565 | 2,230,326,824.6 | 13.37 biliioni |
| 12 | SASA Stell Rolling | 100,000,000 | 11,619,125 | 88,380,875 | 1,311,572,185 | 7.86 bilioni |

**Chanzo, taarifa ya CIS Wizara ya Fedha, 2011**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuiagiza Wizara ya fedha kutayarisha orodha ya madeni inayozingatia malimbikizo ya riba ili Wizara ya fedha ilikaidi hivyo kipengele cha *compound interest* kimekokotolewa na wataalamu wa Kamati na kuonyesha hali halisi ya deni ilivyo hivi sasa ni shilingi **trilioni 1.4**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashangazwa na kusikitishwa na jitihada dhaifu za ukusanyaji wa madeni haya huku Serikali ikiendelea kutoza kodi wananchi masikini, na kuachia zaidi ya shilingi **trilioni 1.4** ikiwa ni fedha za umma kumilikiwa na watu wachache kinyemela.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya kampuni zinazodaiwa kulipa kwa kusuasua na zingine kukaidi kulipa zina uwezo, zinafanya kazi na biashara kwa faida na zina dhamana ambazo zinashikiliwa na Serikali. Mfano uwezo wa mmiliki wa makampuni ya *21st centuries Textile Industries Ltd* na Mohammed Enterprises unafahamika.

**Mheshimiwa Spika,** inashangaza kwa kampuni hizi kukaidi kulipa deni lake lililofikia shilingi **bilioni 5.04.** Vilevile mmiliki wa kampuni za *Farm Equip (T) Ltd* na *Quality Group Garage* zimekuwa zikiendelea kukaidi kulipa deni lake lililofikia shilingi **bilioni 9.06**, aidha, kampuni ya ALAF inadaiwa shilingi **bilioni 13.37**.

**Mheshimiwa Spika,** hii ni baadhi tu ya mifano iliyoko kwenye orodha ndefu ya madeni ya *Commodity Import Support*-CIS. Vile vile, Kamati ina taarifa kwamba, kuna mfanya biashara maarufu hapa nchini ambaye alilaghai zaidi ya kampuni 31 na kujichotea mabilioni ya fedha kwa makubaliano kuwa ataweza kuirithi mikopo hiyo, lakini badala yake ameitelekeza mikopo hiyo na kuibua malalamiko makubwa kutoka kwa wafanyabiashara wenzake.

Kamati inahoji ***Ni nini kilichoifanya Serikali ishindwe kukusanya madeni haya kwa muda mrefu?*** Serikali inatakiwa kufanya uamuzi wa dhati kutumia sheria kali kama kukamata mali za wadaiwa na kuwakamata wale waliodanganya na kisha kuwafikisha katika vyombo vya sheria

## 2.7 Mgogoro wa Vodacom (T) Ltd na Shivacom (T) Ltd

**Mheshimiwa Spika,** kampuni ya Vodacom na Shivacom ziliingia mkataba wa kibiashara mwezi Julai, 2007 ambapo kampuni ya Shivacom ilitakiwa kuzalisha vocha za simu kwa ajili ya kampuni ya Vodacom. Hata hivyo kampuni ya Vodacom ilibainika kuwa kampuni ya Shivacom ilikuwa ikifanya udanganyifu kwa kuzalisha vocha pacha na kuzipeleka moja kwa moja sokoni na zingine zinazofanana na zilizopelekwa sokoni zilipelekwa kampuni ya Vodacom ambao baada ya kuziuza wateja walikuwa wakilalamikia kuuziwa vocha zilizokwisha tumika. Kutokana na hali hii kampuni ya Vodacom iliamua kuvunja mkataba na Shivacom mwezi Julai 2012.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mkataba kati ya Vodacom na Shivacom kuvunjika, mambo yafuatayo yalitokea:-

1. Kwa kipindi cha miaka mitano vocha zilizouzwa na kampuni ya Shivacom ziliuzwa bila kulipiwa kodi ya Serikali kwani kampuni iliyopaswa kulipa kodi husika ni Vodacom.

2. Wananchi walionunua vocha kutoka Vodacom walipata hasara kwa kununua vocha ambazo zilikuwa hazina manufaa kwao.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mazingira hayo, Kamati iliiomba Wizara ya fedha kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufanya utafiti ili kubaini kiasi cha kodi ya Serikali kilichopaswa kukusanywa kutokana vocha pacha zilizouzwa bila kupitia kampuni ya Vodacom na kutaka Kamati ipewe taarifa hiyo katika vikao vya Kamati kuanzia tarehe 4-8 Mei, 2015.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa ukaguzi wa awali uliofanywa na TRA, Vodacom imekuwa ikiingia

mikataba na makampuni ya ndani na nje ya nchi ili kutengeneza vocha za muda wa maongezi kwa kiwango mbalimbali. Katika mkataba kati ya Vodacom na Shivacom ilikubaliwa kuwa Shivacom watengeneze vocha za shilingi 500/= na shilingi 2,000/= na kulipwa na Vodacom ada ya shilingi 20 kwa vocha ya shilingi 500 na shilingi 80 kwa vocha za shilingi 2,000 (yaani 4%).

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa utekelezaji wa makubaliano hayo ya kibiashara, Vodacom imedai ilikuwa ikipata malalamiko toka kwa wateja waliokuwa wakishindwa kuingiza namba za siri za vocha kwenye simu kwa kukataliwa na mitambo ya Vodacom maana mitambo huonyesha vocha imeshatumika. Hivyo, mnunuzi wa vocha (*subcriber*) hurudi kwa muuzaji (wakala mdogo) na kuomba arudishiwe pesa yake. Wakala mdogo naye huomba kurudishiwa fedha toka kwa wakala mkubwa, ambaye naye kurudisha vocha kwa Vodacom na kuomba kurudishiwa fedha aliyotumia kwenye manunuzi. Vodacom hutoa '*credit notes*' baada ya kujilidhisha na malalamiko hayo. Kwa mujibu wa Vodacom, tatizo hili lilianza kugundulika kuanzia mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa na vielelezo vilivyotolewa na Vodacom kwenye vikao vya pamoja kati ya uongozi na maofisa wa TRA kwa nyakati tofauti ilielezwa kuwa tangu mwaka 2009 hadi 2012, Vodacom ilirudisha kiasi cha shilingi **74,343,903** (ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani) kwenda kwa wateja walionunua vocha za shilingi 500 ambazo walizirudisha kwa mawakala waliokuwa wamewauzia. Hivyo kwa mujibu wa Vodacom, vocha zilizohusika na upotevu huu zina thamani ya shilingi **74,343,903.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwamba kiwango hicho cha hasara kinaweza kuwa siyo sahihi kwa sababu upo uwezekano mkubwa kuwa wateja wengine walionunua vocha halali na kushindwa kuzitumia hawakudai marejesho. Katika ukaguzi huo TRA ilibaini kuwa vocha za muda wa maongezi zilizo zilizotengenezwa na Shivacom na kukabidhiwa kwa Vodacom kwa kipindi cha 2007 hadi 2012, zilikuwa na thamani ya shilingi **683,530,000,000/=** (*Face value*-500/=) zilizogharimu shilingi **27,341,200,000/=** yaani shilingi 20/= kwa kila vocha iliyotengenezwa. Na vocha za shilingi 2,000/= zenye thamani ya shilingi **241,804,000,000/=** (*face value*) na ziligharimu shilingi

**9,672,160,000/=** yaani shilingi 80/= kwa kila vocha iliyotengenezwa. Kwa kipindi hichi jumla ya vocha zote zilizotengenezwa zilikuwa na thamani ya shilingi **925,334,000,000/=** (*VAT inclusive*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa zilizotoka kwenye mitandao ya jamii ilielezwa kuwa Vodacom imepata hasara ya shilingi **bilioni 675** na Serikali imepoteza kodi ya shilingi **bilioni 121** kutokana na kuwepo vocha bandia za shilingi 500 "jero jero". Taarifa hizi zikilinganishwa na taarifa ambazo TRA ilipata kutoka Vodacom, vocha za shilingi 500 "jero jero" zilizozalishwa na Shivacom kwa kipindi tajwa zilikuwa na thamani ya shilingi **bilioni 683**, ambazo zinakaribiana na thamani iliyotajwa kwenye mitandao ya jamii.

**Mheshimiwa Spika,** TRA pia ilifanya ulinganifu wa ulipaji wa kodi wa kampuni ya Vodacom kwa kipindi cha mkataba wa Shivacom ili kujilidhisha mwenendo wa ulipaji wa *VAT* na *Excise Duty*, takwimu zinaonyesha kuwa kwa kipindi hicho cha 2008/2009-2011/2012 Vodacom ililipa kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax- VAT*) kiasi cha shilingi **bilioni 118.58** kwa mauzo yake yote. Mauzo ya vocha za 500/= na 2000/=

pekee yalikuwa shilingi **bilioni 925.33** yenye thamani ya kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax*-VAT) ya shilingi **bilioni 166.56** ukiachilia mbali mauzo ya vocha zingine kama zile za shilingi 10,000/=, 5,000/=, 1,000/= na mauzo mengine kwa njia ya mtandao.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa za Vodacom kukinzana na zile za Shivacom pamoja na zile zilizotolewa kwenye mitandao ya kijamii, Kamati iliiagiza TRA kufuatilia na kufanya uchunguzi wa kina (*Forensic Investigation*) ili kubaini usahihi wa taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 17/05/2015 baada ya taarifa ya mgogoro wa Vodacom na Shivacom kuwasirishwa mbele ya Kamati, Kamati ilimwagiza Kamishna Mkuu wa TRA kushughulikia mambo yafutayo na kuwasilisha matokeo yake ifikapo tarehe 01/06/2015:-

1. TRA ifanye ukaguzi na kuthibitisha vocha za shilingi milioni 74 kwa kuziona (*physically*) na kulinganisha na zile halisi.

2. TRA iwatambue wale wote ambao hawaja dai marejesho yao baada ya kununua vocha na kukuta zimetumika.

3. TRA ifanye forensic audit kwenye mitambo ya Shivacom ili kujiridhisha kama walitengeneza hizo vocha za ziada au la, na kuweza kujua idadi.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, ukaguzi huu wa kina bado haujakamilika kutokana na danadana anazopigwa TRA na makampuni ya Vodacom na Shivacom, kwa mfano Vodacom alipoombwa vielelezo vya vocha bandia (*dublicate voucher*) zote zilizouzwa na kurudishiwa fedha na mawakala kuandikiwa '*credit note*' za shilingi **milioni 74,343,903**/= ifikapo tarehe 21 mei 2015. Vodacom waliomba wapewe muda hadi tarehe 25,Mei 2015 na ilipofika tarehe hiyo wakaomba waongezewe muda zaidi hadi tarehe 28,Mei 2015 ambapo walitoa '*credit notes*' pamoja na sampuli ndogo za vocha feki na kupelekwa katika idara ya upelelezi ya TRA kwa ajili ya forensic investigation tarehe 29,Mei 2015. TRA bado hawajaweza kuziona vocha zote feki.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shivacom tarehe 1, Juni 2015 wapelelezi (*Forensic Investigation Officers*) kutoka TRA walitembelea Shivacom kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Tarehe 1, Juni 2015 Shivacom walitoa maelezo kuwa shughuli za kibiashara zilifungwa tangu July, 2012 na wafanyakazi wote walisimamishwa kazi. Kwa maelezo ya Shivacom, mtu pekee anayeweza kusaidia uchunguzi ni Mr. SAnjari Nautiyal, MKurugenzi wa fedha wa *Ultimate Security Ltd*, kampuni tanzu ya Shivacom. Hata hivyo ilielezwa kuwa, Mr. Sanjari sasa yupo India kwa likizo yake ya mwaka na anategemewa kurudi 2 Juni 2015. Shivacom wakapendekeza uchunguzi uanze tarehe 3, Juni 2015.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hali hiyo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

1. Kwa kuwa Vodacom imeweza kutoa *credit notes* ya shilingi milioni 74 na baadhi ya vocha feki Kamati inaamini kuwa kuna kila dalili ya udanganyifu wa vocha feki toka kwa kampuni ya Shivacom.

2. Kutokana na danadana za Vodacom kushindwa kutoa vielelezo vya vocha feki zenye jumla ya shilingi milioni 74 na kwa kuwa Vodacom ilifanya

malipo ya kodi ya VAT kwa kipindi cha mwaka 2008/2009 hadi 2011/2012 ni shilingi bilioni 118 tu wakati thamani ya mauzo kwa vocha za shilingi 500/= na 2,000/= ilikuwa shilingi bilioni 925 yenye thamani ya VAT ya shilingi bilioni 166 bila kuhusisha mauzo ya vocha zingine za shilingi 10,000/=, 5,000/=, 1,000/= na mauzo mengine kupitia mitandao, hivyo huenda kuwa Vodacom inahofia ukaguzi na uchunguzi huu unaweza kuibua mambo mengine ya ukwepaji mkubwa wa kodi.

Hivyo basi, Kamati inaendelea kuiagiza TRA na TCRA kukamilisha uchunguzi (*Forencic investigation*) haraka kabla ya tarehe 20, Juni 2015, ili kujua kiasi halisi cha hasara na kodi iliyo punjwa. Endapo itathibitika kuwa kampuni ya Shivacom ilifanya udanganyifu wa kugushi vocha hizo atawajibika kulipa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kulinganana na thamani ya vocha zilizouzwa na mauzo hayo yatatozwa kodi ya makampuni (*Corporate Tax*) kwa mujibu wa kifungu cha 94(6)(a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004. Na kwa kuwa ni udanganyifu (*fraud*) hatua zingine za kisheria kuhusiana na jinai zichukuliwe.

Kwa upande wa Vodacom, endapo itabainika kuwa kampuni imekwepa kodi italazimika kulipa kodi zote zilizopunjwa kwa kipindi husika.

## 2.8 Mgogoro kati ya Jumuiya ya Wafanya Biashara na Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Wafanya Biashara ilikutana na Kamati kwa nyakati tofauti kuelezea malalamiko yao kuhusu matumizi ya mashine za EFDs na ongezeko la kodi la 100% na kwamba kilio chao hicho kimekuwa hakisikilizwi na Serikali. Kamati ilifanya jitihada na kuwakutanisha Jumuiya ya wafanya biashara na Waziri wa fedha na baade Jumuiya ya wafanya biashara na Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayo furaha kubwa kuliarifu Bunge lako kuwa mgogoro kati ya Serikali na Jumuiya ya Wafanya Biashara umemalizika. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali na Jumuiya ya Wafanya Biashara kwa kushughulikia mgogoro uliokuwepo hadi kukamilika kwake kwa manufaa ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepata taarifa kuwa Kamati ya maboresho ya pamoja iliyoundwa kati ya Serikali na Jumuiya ya Wafanya Biashara imekamilisha kazi yake na kwamba mapendekezo yake yamekubaliwa napande zote mbili na kuandaa Mpango Kazi wa kutekeleza mapendekezo la Kamati.

Kamati ya maboresho imefanya kazi nzuri hasa katika kutatua kero za msingi za wafanya biashara ambazo zilihusu:-

- Ushuru wa forodha;
- Ongezeko la kodi la 100%;
- Gharama za uendeshaji na
- Matumizi ya EFDs.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya mapendekezo 10 yaliyotolewa na Kamati ya maboresho yalikubaliwa na Serikali na Mpango kazi wa Utekelezaji wa mapendekezo umeandaliwa na kukubaliwa **(Angalia Kiambatisho A).**

Baadhi ya mambo ya msingi yaliyokubaliwa ni pamoja na:-

i. Kukosekana kwa uwazi wa kodi na ushuru wa forodha (bandarini) ambapo inapendekezwa kuwepo na uwazi wa kutosha kwenye zoezi zima la uthaminishaji wa bidhaa, na ikiwekezana kuwepo bei elekezi kwa baadhi ya bidhaa ambazo zitakapoainishwa zitalihakikishia Taifa kupata mapato mengi na kwa uhakika zaidi. Hivi sasa maandalizi ya kupanga bei elekezi kwa kutambua bidhaa zinazo husika na zoezi hilo hadi July 15, 2015 itakuwa imekamilika.

ii. Uwepo wa viwango vikubwa vya kodi visivyolipika, Kamati ya maboresho imebaini viwango vya tozo za kodi kwa sasa ni vya juu sana, hivyo Kamati inapendekeza kuwepo kwa maboresho ili viendane na mlinganisho wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi kufikia 01 July, 2015 zoezi hili litakuwa limekamilika.

iii. Matumizi ya mashine za kielekroniki (EFDs), Kamati ya maboresho inashauri uhamasishaji ufanyike sambamba na utatuzi wa changamoto za kimfumo. Aidha wajumbe wa

Kamati watafanya ziara za mafunzo katika nchi mbalimbali zilizofanikiwa katika matumizi ya EFDs (*best practice*), ili kuishauri Serikali namna bora ya matumizi ya mashine za EFDs na ikakubalika kuwa zoezi hili lifanyike na kukamilika kabla ya tarehe 31, Disemba 2015.

Kamati inasisitiza kwamba zoezi hili likamilike kama ilivyokubalika katika Mpango Kazi hatua ambayo itasaidia kuondokana kwa malumbano yaliyokuwepo kwa muda mrefu kati ya Serikali na wafanyabiashara hali iliyopelekea upotevu wa mapato na wakati mwingine kuvunjika kwa amani.

### 2.9 Tathimini ya Mashirika ya Umma yaliyo binafsishwa

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya mashirika 274 yamebinafsishwa kutoka katika sekta za kilimo, viwanda, maliasili na utalii na nishati na madini. Hadi 30, Machi 2014, mashirika yaliyokuwa yamefanyiwa upeLembaji yalikuwa 103 tu kati ya hayo, mashirika yanayofanya vizuri ni 34, yanayosuasua 25 na

yaliyofungwa ni 44. Kwa takwimu hizo ni makampuni 171 bado hayajafanyiwa upelembaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hairidhishwi na hatua zinazochukuliwa na Serikali kufanya tathimini ya mashirika yaliyo binafsishwa. Kwa mfano, kampuni ya *Williamson Diamond Mines* na kampuni zingine na mashirika mengi yamekuwa yakilalamikiwa utendaji wake, pamoja na malalamiko yaliyopo bado Serikali haijaona umuhimu wa kuyafanyia tathimini mashirika na makampuni yanayolalamikiwa. Malalamiko dhidi ya makampuni na mashirika hayo ni pamoja na:-

1. Wawekezaji wengi hawajalipa madeni ya ununuzi wa mashirika hayo kwa serikali, kwani mpaka sasa ni zaidi ya shilingi **bilioni 650** zinadaiwa katika ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

2. Ushauri uliotolewa na timu ya ushauri ya upelembaji haujafanyiwa kazi na Serikali mpaka sasa.

3. Ugumu wa mawasiliano baina ya Serikali na wawekezaji kutokana na baadhi ya mashirika kubinafsishwa muda mrefu na kutokuwepo kwa mawasiliano baina ya Serikali na wawekezaji, kwani wawekezaji wengi wamebadili anwani zao (*Postal and physical address*) na hata umiliki wa mashirika husika hali inayopelekea taarifa zilizopo kuwa tofauti na hali halisi.

4. Katika uchambuzi uliofanywa na timu ya ushauri ya umpelembaji pia kuwa, imeonekana kuwa kuna mashirika na makampuni mengine yamebadilishiwa matumizi tofauti na matakwa ya mkataba.

5. Baadhi ya mikataba kutokuwa na mpango wa uwekezaji, kukosekana/kutokuwepo kwa mikataba ya mauzo.

6. Hakuna ufuatiliaji thabiti wa utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa.

Kamati inashauri kwamba, Msajili wa Hazina afanye tathimini ya mashirika yote yaliyo binafsishwa (hadi Desemba, 2015) na kwamba

makampuni yaliyoshindwa kulipa, yaliyosimama uzalishaji, yaliyobadirisha matumizi kinyume na matakwa ya mkataba, mashirika na makampuni hayo yataifishwe na kurejeshwa Serikalini.

### 2.10 Akaunti za Serikali katika benki za biashara na huduma za bima

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB), Benki ya Posta Tanzania (TPB) na Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ni benki zinazomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moj (100%). Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake imebaini kuwa, Serikali yenyewe haitunzi fedha zake katika benki hizo ambazo inazimiliki kwa 100%. Hali inayopelekea benki hizi kuwa na tatizo kubwa la mtaji. Mbaya zaidi na tena inashangaza hata Wizara ya fedha ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa Benki hizi, Wizara ya Fedha na taasisi zake wanatunza fedha zao kwenye benki zingine za biashara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano, Serikali inatunza fedha zake kwenye benki za biashara zinazomilikiwa na kampuni binafsi zifuatazo:-

- Kenya Commercial Bank Taasisi **(11),**
- Barclays Bank **(14),**
- Bank of India **(7),**
- Stanbic Bank **(39),**
- Standard chartered bank **(56)** n.k, huku benki za Serikali zikiambulia sifuri na kukosa mitaji ya kujiendesha.

**Mheshimiwa Spika,** ni jambo la kushangaza kuwa Serikali iko tayari kutunza fedha zake katika Benki za Kenya, India, Uingereza n.k lakini si benki inazozimiliki yenyewe. Si nia ya Kamati kukataza Serikali kufungua akaunti katika benki mbalimbali za biashara zinazomilikiwa na kampuni binafsi isipokuwa ni lazima kipaumbele kiwe katika benki za Serikali ili kuzipa nguvu zaidi ya kimtaji na kuziwezesha kutoa mikopo zaidi. Ikumbukwe kwamba hatma ya benki hizi za Serikali iko mikono mwa Serikali hivyo ni lazima Serikali iwe na utaratibu wa kupenda na kuthamini mali zake. **(Angalia Kiambatisho B) kinachoonyesha Serikali na Taasisi zake zinavyoyunza pesa zake kwenye benki zinazomilikiwa na watu binafsi)**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile kwa upande wa Bima takwimu zilizowasirishwa kwenye Kamati zinaonyesha kuwa, kwa makampuni 17 ya Bima kiasi cha fedha kilicholipwa na taasisi za umma kwa mwaka 2014 kununua huduma za bima katika makampuni mbalimbali ya bima hapa nchini kilikuwa ni shilingi **bilioni 16.8**. Kampuni ya Bima iliyopata mgao mkubwa zaidi wa bima zilizokatwa na taasisi za umma kwa mwaka 2014 ilikuwa ni *Tan Re* iliyopata 33.8% ya bima zote, ikifuatiwa na kampuni ya Phoenix (28.1%) na *Alliance Life* (15.8%) huku shirika la Bima la Taifa (National Insuarance Company – NIC) ikiambulia kiasi kidogo tu.

## 2.11 Manunuzi ya umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata taarifa juu ya ununuzi wa mabehewa yasiyokuwa na ubora 150, kwa mujibu wa mkataba Mabehewa yaliyo agizwa na *Tanzania Railway Limited* (TRL) ni 274. Aidha uingizwaji wa mabehewa 124 yaliyobaki ulisimamishwa baada kugundulika kuwa mabehewa yaliyokwisha ingizwa hayakuwa na ubora na viwango vilivyokubalika kwenya mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** cha kushangaza zaidi malipo yote kwa ajili ya mabehewa 274 yasiyo na ubora ulikuwa umefanyika tofauti na matakwa ya mkataba ambapo jumla ya shilingi **bilioni 230** zimelipwa. Mkataba unaitaka TRL kulipa 50% kabla ya kuingiza mabehewa, 40% baada ya kuyapokea na 10% baada ya mabehewa kuwa yamefanya kazi ndani ya mwaka mmoja na kudhibitika kuwa yana ubora ulikokuwa unatakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupata taaifa hizi Kamati iliitaka Mamlaka ya Uthibiti wa Manunuzi ya Umma (Public Procurement Regulatory Authority –PPRA) kuwasilisha taarifa ya mchakato wa manunuzi wa mabehewa haya na wakati huo huo Waziri wa uchukuzi akaunda tume ya ukaguzi maalum ya mchakato mzima. Na kwamba taarifa iwasilishwe kabla ya tarehe 11, Mei 2015. Kamati inamshauri Waziri wa uchukuzi kuwasilisha mapema taarifa hii Bungeni ili kuweza kuwabaini watendaji wote waliotekeleza majukumu yao kinyume na mkataba husika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

## 2.12 Mradi wa umeme Singida

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa Singida wa umeme wa upepo ulikubaliwa kupata mkopo kutoka katika benki ya Exim ya China tangu februari 2014 wa Dola za kimarekani **milioni 136**. Kamati inasikitika kuona kuwa hadi leo Wizara ya Fedha (Hazina) imeshindwa kukamirisha mkopo huo licha ya mkopo huo kupitia hatua zote pamoja na maelekezo ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Maendeleo la Taifa (*National Development Cooperation*-NDC) ndio wahusika wa mradi huu, baada ya kukamilisha taratibu zote zinazohusu mikopo kwa ajili ya mradi huu ilipeleka maombi yake Serikalini-Wizara ya fedha na kupitishwa na Kamati husika ya madeni ya Taifa. Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliwasilisha maombi hayo katika Benki ya Exim ya China ya jumla ya Dola za marekani **millioni 136** tu, kwa ajili ya mradi tajwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Exim ilihakiki mradi huu na kuupitisha kwa ijili ya kuwapatia NDC mkopo tajwa. Masharti ya awali ya mkopo huo yalikuwa riba ya 1% tu na kulipwa kwa muda wa miaka 25. Hata hivyo kuchelewa kwa kukamilishwa taratibu za mkopo huo kumeathiriwa na mabadiriko ya sera ya mkopo katika

benki ya Exim ambapo riba sasa itakuwa 2% ya utalipwa kwa muda wa miaka 20.

Hata hivyo wataalamu wa NDC wamethibitisha kuwa masharti haya mapya hayataathiri utekelezaji wa mradi na NDC inao uwezo wa kulipa mkopo huo bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia unuhimu wa mradi huu ambao unatarajiwa kuzalisha MW 300 za umeme kwa kutumia upepo huko Singida, na unatekelezwa chini ya mpango wa matokeo makubwa sasa (*Big Results Now*- BRN). Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inakamilisha utaratibu wa kuupata mkopo huu mapema iwezekanavyo kabla masharti hayajabadirishwa tena na hivyo kukwamisha utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa mradi huu na kwa sababu utekelezaji wa kupata mkopo umekuwa wa kusuasua tarehe 28, Machi 2015 Waziri Mkuu alilazimika kuwamndikia barua Waziri wa fedha Saada Mkuya, (Mb) akimtaka akamilishe utaratibu wa kupata mkopo huu mapema iwezekanavyo kabla ya masharti hayajabadirishwa tena na mradi huu ukashindikana kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pia iliiomba kupata taarifa ya hatua zilizofikiwa katika mkopo huo na kuelezwa kuwa Wizara ya Fedha iliwaomba uongozi wa Benki kuwasilisha rasimu ya mkataba wa mkopo wa masharti nafuu ili Serikali kupitia Wizara ya fedha iweze kuchukua mkopo huo mapema na kwamba hadi sasa Benki hiyo bado haijawasirisha rasimu ya mkataba huo kama ilivyo ombwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Viwanda na Biashara alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa  Mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa wizara yake  aliliambia Bunge kuwa, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kupata mkopo wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** kilichoishangaza zaidi Kamati ni barua ya Waziri wa Fedha ya tarehe 26, Machi 2015 akimwandikia *Mr.* Liu Liange *The President of The Export-Import Bank of China*, akimueleza kuwa Tanzania ilishindwa kupata mkopo kutoka china kutokana na mabadiriko ya riba na muda wa kulipa mkopo. Na kwa sababu hiyo, akatuma miradi mipya mbadala itakayo tekelezwa katika Mwaka wa Fedha

2015/2016 huku akiuondoa mradi wa Umeme wa Upepo Singida katika orodha.

**Mheshimiwa Spika,** inawezekanaje na je Waziri wa fedha ana mamlaka gani ya kuondoa mradi wa umeme Singida bila ya Waziri Mkuu kujua?, bila ya Waziri wa Viwanda na Biashara kujua hali Serikali ni moja?. ***Je Bunge lishike lipi kwamba Serikali ya china haijawasilisha rasimu ya mkataba ya mradi huu au Serikali ya Tanzania imeamua kuufuta mradi huu?***

### *2.12 Uhamishaji wa Fedha Haramu (Ilicit Financial Outflow)*

**Mheshimiwa Spika,** Taifa limekuwa linakosa fedha na raslimali za kutoa huduma kwa wananchi wake na kuwekeza kutokana na utoroshaji mkubwa wa fedha na raslimali unaofanywa na baadhi ya makampuni, watu na watumishi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa utafiti wa *Global Financial Integrity* (GFI, Mei 2014), Tanzania iliongoza kwa kuwa na uzoefu wa uhamishwaji wa fedha

haramu ambao unakadiriwa kufikia wastani wa shilingi **trilioni 3.74** (**USD 1.87 billion**) ikilinganishwa na Mozambique (**USD 0.59 billion**), Uganda (**USD 0.88 billion**), Ghana (**USD 1.44 billion**), Kenya (**USD 1.51 billion**) n.k

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa nchi hupoteza mapato ya ya kodi ya shilingi bilioni 498 (**USD 248 million**) 7.4% ya mapato ya Serikali. Kwa Mujibu wa **Report of the High Level Panel on Illicit Financial Flows from Africa by** Thabo Mbeki, kuwa wastani wa **USD 50 Billion** hutoroshwa nje ya bara la Afrika kila mwaka ikiwa Tanzania inapoteza zaidi ya 2% ya GDP. Kwa mujibu wa matokeo ya tafiti hizi Tanzania inaathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na zoezi hili la utoroshaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na tatizo la utoroshaji wa fedha nje ya nchi, Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali ihakikishe inachukua hatua mahususi juu ya kuzuia upotevu huu mkubwa wa fedha. Aidha, Kamati inashangazwa na hatua ya Serikali kuendelea kuwalinda watanzania waliotorosha fedha nje ya nchi hadi kushindwa kuwasilishwa Bungeni kwa kwa taarifa ya mabilioni ya Uswiss.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazo taarifa za uhakika kwamba uandaaji wa taarifa hiyo umekamilika toka mwaka jana. Kamati inashangaa kwanini kumekuwa na kigugumizi kwa Serikali kutoa taarifa juu ya wahalifu hao?.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ankara zisizo sahihi za uuzwaji nje wa bidhaa, eneo la gharama za juu kupita hali halisi (*over-invoicing*), Tanzania iliongoza kwa kupokea **billioni dola 1.03** ikifuatiwa na Ghana **dola 0.27 bilioni**, Mozambique **dola 0.08** na mwisho Uganda **dola 0.05 bilioni**. Kwa upande wa Tanzania bidhaa inayoongoza kwa kuuzwa nje ni madini ya aina mbalimbali asilimia kubwa ikiwa ni dhahabu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ankara zisizo sahihi za uingizwaji ndani wa bidhaa eneo la ankara zilizo juu zaidi ya hali halisi Tanzania iliongoza kwa kutoa dola **0.83 bilioni** ikifuatiwa na Uganda dola **0.81 bilioni,** Ghana dola 0.22 bilioni, Mozambique dola **0.12 bilioni** na Kenya **dola 0.04 bilioni.** Kwa upande mwingine wa akara zisizo sahihi za uingizwaji ndani wa bidhaa eneo la ankara zilizo chini zaidi ya hali halisi Ghana iliongoza kwa dola **0.46 bilioni** ikifuatiwa na Kenya dola **0.44**

**bilioni,** Mozambique dola **0.25 bilioni**, Tanzania dola **0.01 bilioni** na mwisho Uganda ambayo ilikuwa na sufuri. Kwa upande wa Tanzania bidhaa inayoongoza kwa uingizwaji ni mafuta ya aina mbalimbali kwa ajili ya mitambo, majenereta na magari.

***Mheshimiwa Spika, kamati inapenda kufahamu ni kwanini taarifa ya mabilioni ya Uswiss hadi leo haijawasilishwa Bungeni?*** Ni lazima Serikali ionyeshe nia yake thabiti ya kushughulikia tatizo hili na kuhakikisha kuwa inachukua hatua mahususi juu ya kuzuia upotevu huu mkubwa wa fedha za umma na kwamba wale wote waliohusika na utoroshaji wa fedha wanazirejesha, aidha kwa hiali au kwa kuzuia akaunti zao.

**2.13 Diplomasia ya Kiuchumi**

**Mheshimiwa spika,** pamoja na kazi kubwa inayofanyika kupitia diplomasia ya kiuchumi. Kamati ilipofanya ziara mbalimbali za kikazi nje ya nchi ilibaini udhaifu uliopo katika kuunganisha jitihada zinazofanywa na Waheshimiwa Mabalozi. Kufuatia changamoto hiyo, Kamati inashauri uandaliwe utaratibu mzuri wa kuwakutanisha Waheshimiwa

Mabalozi, Serikali na Waheshimiwa Wabunge katika kila Mwaka wa Fedha ili kubadilishana mawazo na kuwa na mkakati wa pamoja wa kutumia fursa zilizopo na zinazojitokeza.

**Mheshimiwa spika,** Kamati pia inashauri kwamba ni vyema kama nchi tuwe na sera nzuri kwa ajili ya watanzania waishio nje ya nchi ili kurahisisha utumaji wa fedha na uwekezaji nchini. Mfano, kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu zinaonyesha kuwa shilingi **bilioni 500** (USD 250 million) kila mwaka hutumwa kutoka nje ya nchi (remittance). Ikilinganishwa na nchi ya Kenya ambapo wakenya walioko nje ya Kenya hutuma USD 1445 Millioni (sawa na **shilingi trilioni 2.89**) hii ni tofauti kubwa sana na hivyo tunahitaji kuwa na sera na sheria thabiti za Diaspola kwani nchi jirani ya Kenya wana *National Diaspola Policy* na *National Diaspola Act* ambayo imesaidia kuongeza fedha za kigeni kwenye pato la Taifa la nchi hiyo.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 4.1 WIZARA YA FEDHA- FUNGU 50

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Fedha na Taasisi ziliuzo chini yake zinaomba kuidhinishiwa takriban Sh. **60,594,649,000 :00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Sh. **5,602,326,000:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara na Sh. **54,992,323,000:00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **370,544,428,800:00.** Kati ya fedha hizo, Sh, **12,000,000,000:00** ni fedha za ndani na Sh. **358,544,428,000:00** ni fedha za nje.

## 4.2 OFISI YA MSAJILI WA HAZINA – FUNGU 7

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **27,257,674,000:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Sh. **2,649,137,000:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara na Sh. **24,608,539,000:00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Ofisi ya Msajili wa hazina inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **999,885,000:00.** Kati ya fedha hizo, Sh, **650,000,000:00** ni fedha za ndani na Sh. **349,885,000:00** ni fedha za nje.

## 4.3 TUME YA PAMOJA YA FEDHA – FUNGU 10

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Tume ya Pamoja ya Fedha inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **1,966,073,000:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Sh. **431,328,000:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara na Sh. **1,534,745,000:00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, maombi haya ya fedha za za matumizi mengineyo ni pungufu kwa asilimia 19.2 ya bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ya sh. **1,900,000,000:00**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Tume ya Pamoja ya Fedha - Fungu 10 haikuombewa fedha yoyote kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

## 4.4 KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU – FUNGU 13

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kinaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **1,534,745,000:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa vitengo vyote vilivyo chini ya Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kinaomba kuidhinishiwa fedha za ndani jumla ya Sh. **35,768,000:00**.

## 4.5 WIZARA YA FEDHA FUNGU 21- HAZINA

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Fedha - Hazina inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **263,453,401,000:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Sh. **3,599,230,000:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara na Sh. **529,854,171:00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Fedha – Fungu 21 Hazina inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.

**680,960,366,000:00.** Kati ya fedha hizo, Sh, **671,926,000,000:00** ni fedha za ndani na Sh. **9,034,366,000:00** ni fedha za nje.

**IDARA YA MHASIBU MKUU- FUNGU 22- DENI LA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Idara ya Mhasibu Mkuu – Deni la Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **6, 522,875,655,000:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, **Sh. 8,218,655,000:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara . Aidha, Sh. **6,514,657,000,000: 00** kwa ajili ya kulipia deni la Taifa.

**4.6 IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI - FUNGU 23**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **87,358,063,800:00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Sh. **6,851,914,800:00** ni kwa ajili ya matumizi ya kulipia mishahara kwa Watumishi wa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Sh. **80,506,149,000:00** zinaombwa kwa ajili kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali – Fungu 23 inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. **4,673,845,,000:00.** Kati ya fedha hizo, Sh, **3,000,000,000:00** ni fedha za ndani na Sh. **1,673,845,000:00** ni fedha za nje.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbali mbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia kuiongoza Kamati. Na pia, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb. M/Kiti
2. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb. MM/Kiti
3. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb.

4. Mhe. Shawana Bukhet Hassan, Mb.
5. Mhe. Mohamed Hamis Misanga, Mb.
6. Mhe. Josephine J. Genzabuke, Mb.
7. Mhe. Hussein Nassor Amar Mb.
8. Mhe.Ahmed Juma Ngwali, Mb.
9. Mhe. Joyce John Mukya, Mb.
10. Mhe.David Zakaria Kafulila, Mb.
11. Mhe.Said Mussa Zuberi, Mb.
12. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, Mb.
13. Mhe. Dkt. Telezya Luoga Huvisa, Mb.
14. Mhe. Vicky Pascal Kamata, Mb.
15. Mhe. Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mb.
16. Mhe. Khatibu Said Haji, Mb.
17. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, Mb
18. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
19. Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb

Aidha, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha Mhe. Saada S. Mkuya (Mb), Naibu Mawaziri wa Fedha Mhe. Mwigulu L. Mchemba (Mb) na Adam K. Malima (Mb) , Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote

zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na Katibu wa Bunge Dkt Thomas Kashillilah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuwashukuru Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Angela Shekifu, Makatibu wa Kamati hii kwani sote kwa pamoja tumeweza kukamilisha maandalizi ya Makadirio haya kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**Mhe.Luhaga Joelson Mpina (Mb)**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA**
07 Juni, 2015